


Utiaji saini ujenzi wa miradi ya maji ya miji 28, Ikulu Chamwino jijini Dodoma



“ Tukio hili la kusaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji ya miji 28 linaenda kutatua kero za wananchi.

“Mageuzi Yanaendelea Wizara ya Maji” Aweso

Nawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya.



Serikali tunatekeleza huduma muhimu kwa wananchi kwa fedha zetu, pia kushirikiana na wadau wa maendeleo. India wamekuwa washirika wetu wakubwa katika Sekta ya Maji

Utiaji saini ujenzi wa miradi ya maji ya miji 28, Ikulu Chamwino jijini Dodoma



MHE. SAMIA SULUHU HASSAN RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

“Tukio hili la kusaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji ya miji 28 linaenda kutatua kero za wananchi.

Nawashukuru viongozi na watumishi wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Serikali tunatekeleza huduma muhimu kwa wananchi kwa fedha zetu, pia kushirikiana na wadau wa maendeleo. India wamekuwa washirika wetu wakubwa katika Sekta ya Maji

Mradi huu ni matokeo ya ushirikiano wa dhati kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya India. Miji yote 28 itanufaika na hakuna mji utakaoachwa

Wizara ya Maji mmebadilika sana, sasa tunakwenda vizuri. Jipangeni katika usimamizi wa wakandarasi na miradi ili maji yapatikane. Serikali itaendelea kujenga miradi ya maji kila kona ya nchi yetu

Mradi wa maji wa Same-Mwanga ulikuwa na tatizo la kisheria na tumelimaliza, hivyo hadi mwakani maji yapatikana. Tunaenda kutafuta fedha kukamilisha kukamilishi jambo hili

Sekta zetu zishirikiane ili wananchi wafaidike na kazi tunazozifanya.” Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



“Sisi tutahakikisha Watanzania wanapata huduma ya majisafi na ya kutosheleza. Hatutakuwa na nafasi kwa yeyote atakayetaka kutukwamisha

Tunawashukuru sana ndugu zetu, Serikali ya India kwa kufanikisha jambo hili la ujenzi wa miradi ya maji katika miji 28, tunasema akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki” Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso (Mb)



“Serikali ya Tanzania na Serikali ya India kupitia Benki ya Exim India kwa mkopo wenye masharti nafuu tunaenda kutekeleza miradi ya maji ya miji 28, na itaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa asilimia nane.

Thamani ya miradi ya maji ya miji 28 ni Dola za Marekani milioni 500 na mkataba wa kifedha uliingiwa mwaka 2018

Kwa upande wa Tanzania bara thamani ya miradi ni USD milioni 465 na Zanzibar ni USD milioni 35.

Leo tunasaini mradi mkubwa kuliko yote iliyowahi kutekelezwa Tanzania bara, zaidi ya shilingi trilion 1.7. Hivyo, tunawaelekeza wakandarasi kuzingatia ubora, muda na gharama. Mradi ufanikishwe kwa gharama nafuu”

“Mageuzi Yanaendelea Wizara ya Maji” Aweso

Wizara ya Maji inaendelea na mageuzi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma ya maji inaendelea na utekelezaji wa miradi mipya unafanyika kwa kasi kubwa ili wananchi waendeleo kuboresha maisha yao kiuchumi na kijamii kupitia uwepo wa rasilimali maji za kutosha.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema hayo Juni 30, 2022 wakati akizindua Bodi ya Nne ya Maji ya Taifa jijini Dodoma.

Ameainisha jitihada zilizofanyika ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kijiditali wa kukusanya na kuhifadhi takwimu za maji ambao unaitwa Maji-App, kuanzisha Design Manual ili kuhakikisha kuwa gharama za miradi inayoendana hazitofautiani sana, kuanzisha matumizi ya dira za kulipia kabla (prepay meters) ili kupunguza malalamiko ya wateja wa maji yanayohusu usomaji usio sahihi, kukijengea uwezo Chuo cha Maji ili kiweze kuzalisha Wataalam wa kutosha na kukwamua miradi chechefu 126 kati ya miradi 177 iliyokuwa ikisimamiwa na Halmashauri za Wilaya kabla ya kuanzishwa kwa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Waziri Aweso amesema kupitia taftishi iliyofanywa na Wizara ya Maji, ilionekana kuwa rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali nchini kwa mwaka zilizopo juu ya ardhi zinakadiriwa kufikia wastani wa mita za ujazo bilioni 105 na mita za ujazo bilioni 21 zipo chini ya ardhi na hivyo kufanya jumla ya rasilimali za maji nchini kufikia mita za ujazo bilioni 126.

Amesema kiasi hicho cha rasilimali za maji kinaonekana kuwa kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa kuzingatia makadirio ya idadi ya watu milioni 55.9 kwa mwaka 2019.

“Kiasi hiki cha maji kwa mtu kwa mwaka kimepungua kutoka wastani wa mita za ujazo 12,600 mwaka 1960 wakati nchi yetu ikiwa na idadi ya watu milioni 10. hadi wastani wa mita za ujazo 2,250 kwa mwaka 2019” Waziri Aweso amesema na kuongeza pamoja na jitihada zinazofanyika ziko changamoto ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi; kuongezeka kwa mahitaji ya maji kunakosababishwa na kuboreka kwa maisha, kuongezeka kwa viwanda na shughuli nyingine za kiuchumi, kuongezeka kwa idadi ya watu; uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu na matumizi ya maji yasiyo na ufanisi, hususani kwenye kilimo cha umwagiliaji, hivyo kuchangia katika kupunguza kiasi cha upatikanaji wa maji.

Waziri Aweso amesisitiza baada ya Sensa ya Watu na



Makazi mwaka huu, takwimu za upatikanaji wa maji zirejewe ili kuendana na wakati, hivyo Bodi ya Nne ya Maji ya Taifa inategemewa kushauri na kuchochea zaidi juu ya kufanya tathmini ya rasilimali za maji juu na chini ya ardhi mara kwa mara ili kuwa na takwimu sahihi kwa nchi ambazo zitaaidia katika ufanyaji wa maamuzi.

Akiongea katika hafa hiyo, Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) ameitaka bodi iliyozinduliwa kufanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi, pamoja na jamii ambako ndipo

kwenye rasilimali za maji zinazotakiwa kuendelezwa kwa faida ya vizazi vya sasa na baadae.

Mhandisi Mahundi amesema bozi izingatie miradi ya utoaji huduma za maji, uendeleu wake unategemea utunzaji wa vyanzo vya maji na usimamizi mathubuti wa rasilimali za maji kwa ujumla.

Bodi ya Nne ya Maji ya Taifa itaongozwa na mwenyekiti wake Katibu Mkuu mstaafu Mhandisi Mbogo Futakambaka, ambaye ni mmbobezi mkubwa katika masuala ya Sekta ya Maji kwa miaka mingi, kama kiongozi na mtaalamu.

Moja ya majukumu ya bodi hiyo ni kutoa ushauri kwa waziri mwenye dhamana ya maji katika masuala yanayohusu uratibu wa sekta mbalimbali katika upangaji na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji na utatuzi wa migogoro ya maji ya kitaifa na kimataifa.

Wizara ya Maji imejipanga kuwafikishia huduma ya maji wananchi walioopo maeneo ya vijijini kwa asilimia 85 na wananchi wanaoishi maeneo ya mijini kwa asilimia 95 ifikapo mwaka 2025.



Bei elekezi ya Maji vijijini yawekwa hadharani



Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA Mhandisi Clement Kivegalo, (kulia) akionyesha kabrasha ambapo RUWASA imeingia mkataba wa kutengeneza Dira za maji za malipo kabla na Taasisi za Elimu ya Juu, ikiwamo Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (Must).

Serikali kupitia Wizara ya Maji imetangaza rasmi bei elekezi kwa gharama za maji vijijini.

Aidha, uchambuzi wa bei za maji umefanyika katika Vyombo vya Watoa Huduma za Maji ngazi ya Jamii na kuzielekeza jumuiya za maji kuzingatia bei elekezi iliyopangwa na kinyume na hivyo hatua zitachukuliwa kwa watakaokwenda kinyume.

Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso (Mb) akiongea katika hafla hiyo jijini Dodoma ameweka wazi bei za kikomo kwa kila ndoo ya lita 20 kuendana na mifumo/nishati inayotumika katika uzalishaji wa maji ambapo Mfumo wa Nishati ya mafuta ndoo ni shillingi 50, Mfumo/Nishati ya Umeme Jua shillingi 30, Mserereko Shillingi 20, Umeme wa TANESCO shillingi 40 na Pam-pu za mkono bei ya shillingi 20.

Amesema bei za ukomo kwa mita ya ujazo itakua shillingi 2,500/= kutoka shillingi 5,000/= ilivyokua na hivyo Bei za ukomo kwa ndoo

ya lita 20 itakua shillingi 50 badala ya shillingi 100 ya awali.

Mhe. Aweso amesisitiza kuwa hii ni dhamira ya dhati ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi ya Wizara ya Maji ni kutekeleza maono hayo kwa kuweka bei rafiki wanazomudu wananchi.

Katika hafla hiyo, Waziri Mhe. Aweso ametoa vifaa vitakavyotumika katika utendaji kazi ikiwamo pikipiki 250 ambapo 145 zilizokwisha tolewa mwaka 2021 hivyo jumla kuwa 395. Pikipiki hizo zinenda kuboresha utendaji kazi kwa wataalamu wote katika ufuatiliaji, usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya sekta ya maji vijijini.





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akiwasilisha hotuba ya bajeti mapema mwezi Mei 2022 ambapo aliomba Bunge kuidhinisha jumla ya Shilingi bilioni mia saba na tisa milioni mia tatu sitini na moja mia sita na saba elfu (709,361,607,000) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2022/23. Kusoma hotuba tembelea tovuti, www.maji.go.tz



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba akiendesha kikao kazi kuhusu maandalizi muhimu ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa, jijini Dodoma



Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba, (watatu kutoka kushoto walio-kaa), akiwa katika picha ya pamoja na wataalamu mbalimbali walioshiriki kikao kazi kuhusu maandalizi muhimu ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa, jijini Dodoma

Mradi wa maji wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu: Maandalizi Yashika Kasi

Mradi wa maji wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu maandalizi yake yameshika kasi ambapo hivi sasa kazi ya kuhamisha maeneo ya maziko ili kupisha eneo la bomba kuu la maji litakaloanzia ziwa Victoria inaendelea.

Kwa mujibu wa mratibu wa mradi huo Mhandisi Mwajuma Waziri, kazi ya kutoa nafasi kupisha utekelezaji wa mradi huo, kwa kuhamisha maeneo ya maziko ni shirikishi na inawahusisha ndugu wa familia wa wapendwa waliohifadhiwa katika maeneo hayo, pamoja na viongozi wa Serikali za Mitaa.

Mhandisi Waziri amesema idadi ya makaburi 78 yanatarajia kuhamishwa, na hadi tarehe 20 Juni, 2022 zaidi ya makaburi 22 yalishahamishwa kwa kushirikiana na familia husika, na viongozi wa Serikali za Mitaa. Makaburi yalihamishwa na mabaki kuhifadhiwa katika maeneo mapya nje ya eneo la ujenzi wa bomba kuu la maji.

“Kila familia iliyoathirika na zoezi hili inapewa asante na serikali, na endapo mabaki hayatapatikana kwa sababu yoyote, ikiwamo kukosea alama za mahali lilipo kaburi, wakati wa ujenzi mabaki yakipatikana basi familia husika itapewa stahiki kama ilivyopangwa na Serikali” Mhandisi Waziri

amewaambia wakazi wa Itilima wakati wa kuhamisha mabaki yaliyopatikana katika moja ya kaburi, na kuongeza zoezi lote linaugharamiwa na Serikali.

Ameongeza kila kaburi litakalochimbwa kutakuwa na timu ya wataalamu wa afya wataokaogua mabaki ili kujiridhisha endapo ni mabaki ya binadamu, ili kuweka uwajibikaji kwa jamii na malipo.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi Mhe. Lupakiyo Kapanga akiongea kuhusu zoezi hili, ameelekeza familia zitoe ushirikiano kwa sababu ni jambo la maendeleo katika jamii. Amesema ni jambo linalokumbusha tukio ambalo limepita, na hatua ya msingi ni familia husika kushirikiana na kuepuka malumbano.

Mzee Saguda Mayenga, ambaye ni mmoja wa kiongozi wa familia iliyohamisha eneo la maziko ameshukuru kwa ushirikiano mkubwa kati ya Serikali na familia yake. Amesema pamoja na kuhamisha eneo la maziko, anahamu ya kupokea huduma ya maji muda ukiwadia.

Mradi wa maji wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Simiyu ni moja ya mradi wa maji utakaoleta mapinduzi makubwa kwa kuwahudumia wananchi, mifugo na kuendeleza masuala ya kilimo.

Tafti za wataalamu wa mazingira, ikiwamo Umoja wa Mataifa zimebainisha kuwa mabadiliko ya hali ya hewa huchukua muda mrefu, na yanaweza kuwa ya asili. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1800 shughuli za kibinadamu zimechangia kwa kiasi kikubwa, ikiwamo mkusanyiko wa gesi ukaa kwenye mazingira.



Imalamate, Mkuu wa Wilaya ya Busega Mhe. Gabriel Zacharia akiongea na wakazi wa Imalamate ambao wamekubali kuhamisha eneo la maziko ili kupisha ujenzi wa mradi wa maji

UZINDUZI WA MRADI WA MAJI WA KYAKA BUNAZI

Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua mradi wa maji wa Kyaka-Bunazi, uliopo Missenyi mkoani Kagera. Mradi umegharimu shilingi bilioni 15.7 na utanufaisha wananchi elfu 65, na ni mradi wa kwanza unaotumia chanzo cha mto Kagera



EWURA GCC YATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA YA SGR



Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Serikali la EWURA (GCC) wakiwa katika ziara ya mafunzo baada ya kuchaguliwa.

Baraza la Ushauri la Serikali la EWURA (GCC), limefanya ziara ya kikazi katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR). Katika ziara hiyo, Baraza limejionea maendeleo ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo kituo cha abiria cha Tanzanite, Pugu pamoja na mitambo ya kupoozea umeme utakao tumika kuendesha treni, katika eneo la Pugu, jijini Dar es Salaam.

Ziara hiyo ya siku mbili ya Baraza ilifanyika Juni 2022 ikilenga kuwapa ufahamu wajumbe wa baraza hilo ambao ndio wameteuliwa, kuhusu shughuli mbalimbali za udhibiti, na kuwaweka katika nafasi nzuri ya kufanya maamuzi katika masuala ya kiudhibiti kwa maslahi ya Taifa.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kaimu mwenyekiti wa Baraza, Mhandisi Lydia Joseph alisema: “Tumeona na kujifunza mengi, ambayo yatatusaidia sana katika kuishauri Serikali katika udhibiti.”



Mstari wa mbele, kushoto ni Kaimu Mwenyekiti wa Baraza Mhandisi Lydia Joseph kutoka Wizara ya Maji.

Wajumbe wengine wanaounda baraza ni Mha. Salum Inegeja (Wizara ya Nishati), Bw. Thabiti Dokodoko (Wizara ya Fedha), Bw. Julius Mwambeso na Bw. Conrad Milinga (Uwekezaji, Viwanda na Biashara).

SERIKALI KUONGEZA UPATIKANAJI WA MAJISAFI KWA KUTUMIA VYANZO TOSHELEVU

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga amesema Serikali imedhamiria kutumia vyanzo vya maji vya mito na maziwa ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Mhandisi Sanga amesema hayo hivi karibuni mkoani Kata-vi akiwa katika ziara ya kikazi mkoani humo.

“Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameleleza Wizara kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wote kwa kutumia vyanzo vya maji vya uhakika ikiwemo mito na maziwa makuu” Mhandisi Sanga alisema na kuongeza wizara inatekeleza kwa kuhakikisha huduma inafika kwa wananchi.

Alibainisha kuwa ziara yake ya kikazi Mkoani humo inafuatia maelekezo ya Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) baada ya kujionea hali ya upatikanaji wa maji alipofanya ziara katika mkoa huu.

“Waziri alipofanya ziara mkoani hapa alielekeza chanzo toshelevu ni Ziwa Tanganyika na kupitia ziara yangu nitatembelea eneo hilo la ziwa na miradi mingine ya maji mkoani hapa kwa lengo la kung’amua namna ya kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi,” Mhandisi Sanga alisema.

Mhandisi Sanga alibainisha mikakati mbalimbali ya Wizara ya Maji katika kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji maeneo mbalimbali nchini mojawapo ikiwa ni hiyo ya kutumia vyanzo toshelevu vya maji.

Alisema mafaniko makubwa yameonekana katika kutumia vyanzo hivyo vikubwa akitolea mfano chanzo cha maji cha Ziwa Victoria ambacho kimekuwa msaada mkubwa kwa mikoa mingi jirani ya Mwanza, Geita, Simiyu, Kagera, Shinyanga na Tabora na lengo ni kufikisha huduma hiyo mkoani Dodoma.

Mhandisi Sanga vilevile alielezea matumizi ya Ziwa Tanganyika ambapo alisema Mkoa wa Kigoma umekwishanza kunufaika na kwamba hatua inayofuatia ni kutumia chanzo hicho kunufaisha maeneo mengine sawa na inavyofanyika katika Ziwa Victoria.

“Ziwa Tanganyika ni chanzo sahihi kwa Mkoa wa Katavi nao kunufaika na huduma toshelevu ya majisafi na salama; ni ziwa lenye kina kirefu na pia halina athari za uchafuzi,” Katibu Mkuu Mhandisi Sanga alisema.

Katibu Mkuu Sanga amefanya ziara ya kikazi mkoani Katavi, pamoja na kuongea na watumishi wa Sekta ya Maji ikiwa ni moja ya matukio ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, ambapo wiki hiyo inatumika kutambua mchango wa Sekta ya Umma katika kuleta maendeleo na mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo.



Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga alipotembelea eneo la Ziwa Tanganyika katika Kata ya Karema Wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi.



Moja ya taswira ya Ziwa Tanganyika linavyoonekana mkoani Katavi. Wizara ya Maji imejipanga kutumia maji kutokakatika ziwa hili ipasavyo, kuwahudumia wananchi. Hayo yamesemwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga wakati wa Wiki ya Utumishi wa Umma 2022



Kitengo cha Mawasiliano
Tovuti: www.maji.go.tz